**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TECHNOLOJIA**

**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**

**CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI ULANGA DVTC**

---

**NDUGU,** ......................................................................................................

YAH: **KUCHAGULIWA KUJIUNGA NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI KATIKA CHUO CHA VETA WILAYA YA ULANGA, MAHENGE - MOROGORO.**

Mkuu wa Chuo Cha VETA Wilaya ya Ulanga anapenda kukufahamisha kwamba umechaguliwa kujiunga na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi VETA Ulanga katika fani uliyoiomba kama inavyoonekana kwenye orodha ya waliochaguliwa inayopatikana kwenye Tovuti ya VETA ya ***www.veta.go.tz.***

Chuo hiki kipo Mkoa wa Morogoro katika Halmashauri ya Wilaya ya Ulanga, kilometre 45 kutoka mji wa Mahenge ambao ndio mji mkuu wa Wilaya ya Ulanga.

**MAAGIZO HAYA YASOMWE KWA MAKINI NA MZAZI/MLEZI NA MWANAFUNZI**

1. Unafahamishwa kwamba umechaguliwa kujiunga na **Chuo cha VETA Wilay ya Ulanga** katika fani ya ...................................... katika hatua ya kwanza (**Level I**), mwaka wa masomo 2026.
2. Mafunzo yatachukua muda wa miaka miwili (2).
3. Chuo kitafunguliwa rasmi tarehe **11 / 01/2026,** fika Bila kukosa.
4. Unatakiwa kuthibitishwa na daktari wa Serikali kuwa unayo afya nzuri ya kumudu mafunzo katika fani uliyopangiwa.
5. Unatakiwa kuthibitisha wewe mwenyewe na mzazi/mlezi/mdhamini wako kwamba umekubali nafasi ya mafunzo uliyopangiwa.

**MUHIMU:**

UNATAKIWA KUJA NA VITU VIFUATAVYO KWA MATUMIZI BINAFSI CHUONI: -

i. Kwa mwanafunzi aliye na **Bima ya Afya** atatakiwa kuionesha mara afikapo Chuoni na kwa asiye nayo atatakiwa kulipa Tsh. **50,400 (atapewa Control Namba ya Bima ya Afya kwa**

**ajili ya malipo hayo)**

ii. Suruali mbili (2) kitambaa cha **ESTEEM No. 1 Dark Blue** zenye upana chini inchi 15 na Turn-up; Marinda mawili kila upande na mfuko mmoja wa nyuma. **(Kama hana atanunua chuoni kwa gharama ya Tsh. 50,000/= zote mbili)**

iii. Kwa wanao vaa hijabu inatakiwa kushonewa kwa kitambaa cha tetron, isizidi setiri ya kifua.

iv. Overall/overcoat moja kwa ajili ya kazi za Vitendo (Practical) yenye rangi ya dark blue. **(Kama hana atanunua chuoni kwa gharama ya Tsh. 40,000/=)**

v. Mkebe (**Mathematical Set - NATARAJI**) kwa ajili ya somo la Michoro ya Kiufundi.

vi. Mashati meupe mawili ya mikono mifupi aina ya TOMATO.

vii. 'Safety Boot' kwa ajili ya karakana na kazi za ufundi.

viii. Mabuti ya Mvua (Gum-boots)

ix. Ndoo mbili ndogo na vifaa vya kulia chakula

x. Ream moja ya Karatasi A4 aina ya **NOPA** au **Mondi Rotatrim**

xi. Fyekeo moja.

xii. Rula pamoja na karamu za kutosha kujifunzia.

xiii. Truck Suit ya Dark Blue yenye mistari myeupe na Raba (**kwa ajili ya michezo**)

xiv. Sweta la rangi ya Dark Blue

xv. Daftari 8 kubwa (Counter Book 3Q)

xvi. Mashuka mawili ya rangi ya Pink kwa wasichana na rangi ya Bluu kwa wavulana, Soksi jozi mbili rangi nyeupe,net ya mbu, ndoo ndogo mbili lita 10, vyombo vya chakula na chai.

**TARATIBBU ZA MALIPO YA SERIKALI:**

Mwanafunzi atapewa Control Namba na Mhasibu wa Chuo kulipia gharama zilizoorodheshwa kwenye majedwali hapo chini: -

| Na | MAHITAJI | IDADI | KIASI | JUMLA | UTARATIBU |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Ada ya Bweni | Mwaka | 120, 000 | 120,000 | Italipwa kwa awamu 2 |
| 2 | Ada ya Kutwa | Mwaka | 60,000 | 60,000 | Italipwa kwa awamu 2 |
| 3 | Fedha ya Tahadhari | Mara 1 | 20,000 | 20,000 | Italipwa anapofungua chuo |
| 4 | Uchakavu wa Godoro | Mara 1 | 5,000 | 5,000 | Italipwa anapofungua chuo |

**MALIPO YA MICHANGO MINGINE YA CHUO:**

| Na | MAHITAJI | IDADI | KIASI | JUMLA | UTARATIBU |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Fedha ya michezo | Mara1 | 15,000 | 15,000 | Italipwa anaripoti chuoni |
| 2 | Fedha ya serikali ya wanafunzi (USO) | Mara1 | 10,000 | 10,000 | Italipwa anaripoti chuoni |
| 3 | Fedha ya Mtihani | Mara1 | 25,000 | 25,000 | Italipwa anaripoti chuoni |
| 4 | Fedha ya mahafali | Mara1 | 15,000 | 15,000 | Italipwa anaripoti chuoni |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 5 | T/Shirt Sare ya Veta | 2 | 17,000 | 34,000 | Inaweza kulipwa kwa awamu 2 |
| 6 | Nembo ya VETA | 2 | 2,500 | 5,000 | Italipwa anaripoti chuoni |

**ANGALIZO:**
Mwanafunzi hatapokelewa chuoni iwapo atafika bila kutekeleza vifungu vilivyotajwa hapo juu. Vile vile kama ataamua kuacha masomo kwa hiari yake, **fedha ikishalipwa hairudishwi.**

**SHERIA, TARATIBU NA MAELEKEZO KWA WANACHUO WOTE**
Ili kufanikisha mafunzo ya ufundi stadi kufanyika kwa ufanisi kila mwanachuo anatakiwa kufuata sheria, taratibu na miongozo mbalimbali ya nchi na chuo. Kutofanya hivyo kunaweza kupelekea hatua mbalimbali za kinidhamu kuchukuliwa dhidi ya mwanafunzi husika. Zifiatazo ni taratibu na sheria za chuo: -

**1. MAHUDHURIO**

a) Kila mwanachuo anatakiwa kufika chuoni kabla ya saa 1:30 asubuhi.
b) Mwanachuo hatakiwi kutoka nje ya chuo kwenda nyumbani, hospitali au sehemu nyingine yoyote kwa sababu ya msiba, kuuguliwa au kuugua ni lazima apate kibali cha Mkuu wa chuo.
c) Mahudhurio chini ya 85% mwanachuo hataruhusiwa kufanya mtihani.
d) Ni marufuku kwa mwanachuo kuingia au kutumia simu ya mkononi sehemu yoyote inayohusiana na mafunzo ikiwa ni darasani au kwenye karakana.

**2. MAVAZI NA USAFI WA MWILI**

a) Mwanachuo unatakiwa kuvaa sare ya chuo ambayo ni suruali ya "Blue" yenye vipimo vilivyothibitishwa na chuo wakati wote unapokuwa katika mazingira ya chuo. Shati jeupe la mikono mifupi lenye Nembo ya VETA lililochomekewa vizuri ndani ya suruali. **Mwanachuo atakayevaa sare ya chuo isiyokidhi vipimo atalazimika kushona au kununua nyingine.**
b) Sare ya chuo itavaliwa wakati wa safari ya kuja chuoni na kurudi nyumbani. Ovaroli litavaliwa wakati wa vipindi vya mazoezi kwa vitendo.
c) Viatu vyenye visingino virefu, kandambili na viatu vya wazi (sandals) haviruhusiwi kuvaliwa chuoni wakati wa mafunzo.
d) Hairuhusiwi kuvaa mapambo ya aina yoyote ile mfano hereni, pete, bangili, mkufu kwa kipindi chote cha mafunzo.
e) Mwanachuo huruhusiwi: kupaka rangi za midomo, kuweka dawa/rangi za nywele, manukato yanayotoa harufu kali, kufuga kucha au kuzipaka rangi, kuvaa bangili, hereni, mkufu, au urembo wowote.
f) Nywele kwa wavulana:
g) Zikatwe ziwe fupi na isiwe kipara. Hairuhusiwi kunyoa mitindo mingine na kufuga Sharubu au Ndevu.
h) Nywele kwa wasichana.
i) Zikatwe ziwe fupi au zisukwe kwa mistari ya kurudi nyuma (twende kilioni). Hairuhusiwi kunyoa au kusuka mitindo nje ya iliyoruhusiwa.

**3. USAFI WA MAZINGIRA YA CHUO.**

a) Mwanachuo unatakiwa kutunza usafi wa mazingira ya chuo ikiwa ni pamoja na kutoandika katika kuta za majengo na kutokukatisha katika sehemu isiyoruhusiwa.
b) Mwanachuo huruhusiwi kubandika tangazo lolote katika kuta na mbao za matangazo, wala kuchora au kuandika kwenye kuta za majengo ya chuo.
c) Vyumba/Madarasa na vifaa vitumiwe kufuatana na shughuli zake, hairuhusiwi kupeleka meza au viti mabwenini.

**4. WIZI, UPOTEVU NA UHARIBIFU WA VIFAA**

a) Vitendo vyovyote vinavyohusisha wizi ni kosa la jinai.
b) Ukipoteza au kuharibu kifaa cha chuo utatakiwa kulipa gharama kamili ya kifaa au ukakinunue kifaa chenyewe.
c) Hairuhusiwi mwanachuo kuingia na kifaa chochote kile kinachofanana na vile vilivyoko ndani ya chuo bila idhini ya Mkuu wa Chuo.
d) Mwanachuo atakaguliwa wakati wa kutoka au kuingai karakana na getini.

**5. UGOMVI:** Kupiga, kupigana na kushambuliana kwa maneno ni makosa ya jinai.

**6. ULEVI:** Mwanachuo haruhusiwi kulewa au kuonekana katika sehemu za vileo, kuvuta bangi au kutumia madawa ya kulevya.

**7. MAPENZI:**

a) Uhusiano wa kimapenzi chuoni kati ya wanafunzi na mwanafunzi au kati ya mfanyakazi na mwanachuo hairuhusiwi kabisa.
b) Mwanachuo yeyote haruhusiwi kuingia maeneo wanayoishi wafanyakazi wa chuo bila kibali au ruhusa.

**8. MIGOMO:** Kushiriki, kushawishi au kuchochea migomo ni kosa la jinai.

**JEDWALI LINALOAINISHA MAKOSA MBALIMBALI NA STAHILI ZA ADHABU ZAKE**

| KUFUKUZWA CHUO | KUSIMAMISHWA MASOMO/KUPOTEZA NAFASI YA BWENI | KUSIMAMISHWA MASOMO/ KUPOTEZA NAFASI YA BWENI |
|---|---|---|
| Wizi, Rushwa na Utapeli | Kukataa adhabu halali | Kuingia maeneo yasiyoruhusiwa. |
| Ulevi, matumizi ya madawa ya kulevya na uvutaji bangi. | Kuharibu mali ya chuo | Kuingia na kifaa chochote kile kinacho fanana na vilivyoko ndani ya chuo bila ruhusa |
| Kupiga au kupigana | Uasherati. | Kupeleka meza au viti bwenini. |
| Kudharau Itifaki za Taifa ikiwepo Bendera ya Taifa, Wimbo wa Taifa, Wimbo wa VETA, n.k. | Kutofanya mitihani/mazoezi bila sababu | Kubandika tangazo lolote katika kuta na mbao za matangazo, kuchora au kuandika kwenye kuta za majengo ya chuo. |

| | | |
|---|---|---|
| Kugoma, kuchochea na kuongoza mgomo, kuvuruga amani na usalama wa chuo na watu. | Kufanya biashara na kujihusisha na siasa chuoni | Kutotunza usafi wa mazingira ya chuo |
| Kufanya jaribio lolote la kujiua/kuua | Kuingia na mgeni/kumkaribisha mgeni bwenini. | Kukatisha katika sehemu isiyoruhusiwa. |
| Kushiriki vitendo vya ugaidi. | Kutumia vifaa visivyoruhusiwa bwenini. | Kutozingatia usafi binafsi wa mwili. |
| Utoro uliokithiri. | Kulala nje ya chuo bila ruhusa ya Mkuu wa Chuo. | Kutoka nje ya chuo bila ruhusa. |
| Kumlaza mgeni bwenini. | Kutumia lugha ya matusi na makelele Bwenini | Kuchelewa kuripoti chuoni kabla ya 1:30 asubuhi. |
| Kupika chakula na kutumia Heater Bwenini | Kutoka nje ya chuo bila sare ya chuo | Kupoteza kifaa cha chuo |

VOCATIONAL EDUCATION TRAINING AUTHORITY
P. O. Box 63
MAHENGE
ULANGA DVTC

Eng. Benitho J. Kigava
**KAIMU MKUU WA CHUO**
**Simu: 0785 479 060**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TECHNOLOJIA**

**MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI**

**CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI ULANGA DVTC**

---

**VOCATIONAL EDUCATION AND TRAINING AUTHORITY MEDICAL EXAMINA**

**Date:..........................................**

The Medical Officer

..................................................................................................................................

..................................................................................................................................

**REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION**

Name of Trainee: ....................................................

Please examine the above named trainee to his/her fitness to undergo training

subsequently work as a/an..........................................................

i. Hearing .....................................

ii. Eyesight ....................................

iii. Asthma.....................................

iv. Other serious disease .......................................

**MEDICAL CERTIFICATE**

I have examined the above named and consider that he/she is physical fit/unfit for training as above.

Date:.......................................... Designation:..................................................

Signature & Official Stamp.......................................................

# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TECHNOLOJIA

## MAMLAKA YA ELIMU NA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

## CHUO CHA MAFUNZO YA UFUNDI STADI ULANGA DVTC

---

### FOMU YA KUKUBALI NAFASI YA MAFUNZO YA UFUNDI STADI

**a) MWANACHUO**

Mimi ........................................................................................ ninakubali

nafasi ya mafunzo katika fani niliyopangiwa, pamoja na kuzingatia sheria na

kanuni za chuo.

**Sahihi ya Mwanachuo ..................................Tarehe .................................**

**b) MZAZI/MLEZI/MDHAMINI:**

**Mimi..................................................... Mahusiano.................................**

**Wa S. L. P. .................................. SIMU ...................................**

Ninathibitisha kuwa ninamdhamini aliyetajwa hapo juu na nitamlipia gharama zote za mafunzo (Ada) pamoja na nauli wakati wote wa kwenda na kurudi nyumbani kwa likizo na baada ya mafunzo ya awali.

**Sahihi ya mdhamini.............................. Tarehe ...............................**